



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU

Namba ya Zabuni: LGA/061/2023-2024/NC/01


Kwa ajili ya: UWAKALA WA UKUSANYAJI ADA YA TAKA NGUMU NA UZOAJI  
TAKA NGUMU NA KUFANYA USAFI KWA MWAKA WA FEDHA 2023-2024

Tarehe: 31 Agosti 2023

Kwa: **WAZABUNI**

1. Halmashauri ya wilaya mbulu katika mwaka wa fedha 2023/2024 inakusudia kutoa **KAZI YA UKUSANYAJI WA ADA YA UZOAJI WA TAKA NGUMU NA UZOAJI WA TAKA NGUMU NA KUFANYA USAFI** katika miji midogo ya Dongobesh, Maghang na Haydom kuanzia mwezi Septemba 2023 hadi mwezi Juni 2024. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu anawatangazia wananchi, vikundi, makampuni na Taasisi mbalimbali kuleta maombi ya Utoaji wa huduma hiyo.
2. Waombaji wa zabuni wanapaswa kutambua kuwa majukumu yao yatakuwa kukusanya ada ya uzoaji taka ngumu toka kwa wananchi kwa kutumia POS zilizounganishwa na mfumo wa TAUSI na kuziwasilisha Halmashauri kulingana na Masharti ya Mkataba. Vilevile wakala atapaswa kuzoa taka na kufanya usafi katika miji ya Haydom, Maghang na Dongobesh.
3. Wakala atapaswa kuonesha umiliki wa magari na/mitambo ya uzoaji taka ngumu katika maeneo yaliyoainishwa hapo juu.
4. Wakala atapaswa kuwa na vibarua wa kutosha wa kufanya usafi katika miji hiyo. Aidha gharama za vibarua zitalipwa na wakala
5. Mwombaji atainisha mchanganuo wa mapato na matumizi, vilevile mwombaji atataja kiasi cha asilimia atakacholipwa kwa mwezi.

6. Koteheni inapatikana kwa kulipa ada ya shilingi 100,000 (Mia moja elfu tu) kwa kila kotesheni. Nyaraka za kotesheni zinapatikana kwenye ofisi ya manunuzi na ugavi, Halmashauri ya wilaya ya mbulu.
7. Zingatia kuwa fomu ya maombi ya kotesheni inajazwa na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria (Power of Attorney) katika kotesheni hii.
8. Mwombaji awasilishe kotesheni halisi na nakala mbili
9. Zabuni ijazwe vizuri, iwekwe kwenye bahasha iliyofungwa kwa Lakiri baada ya kujazwa na wakotesheni na juu ya bahasha iandikwe kwa **HERUFI KUBWA KOTESHENI ILIYOOMBWA** bila kuwekwa alama yoyote ya kumtambulisha muombaji.
10. Zabuni zote zikiwa zimejazwa kikamilifu ziwasilishwe kwa **KATIBU WA BODI YA ZABUNI, HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU, S.L.P 74, DONGOBESEH-MBULU** kabla ya SAA 4:00 asubuhi tarehe 07.08.2023 Ufunguzi wa Zabuni hizo utafanyika katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilishwa Zabuni
11. Zabuni au sehemu za Zabuni ambazo zitawasilishwa kwa kuchelewa au zilizowasilishwa katika muundo usiokubalika hazitakubaliwa wala kuzingatiwa kwa ajili ya tathmini, bila kujali mazingira yoyote

  
Abubakar A. Kuuli  
**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU**

**MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**MBULU**